



TAARIFA KWA UMMA

KURUHUSU LESENI NA RATIBA ZA MABASI 35 YA *KILIMANJARO TRUCK COMPANY LIMITED* KUENDELEA KUTUMIKA

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilitoa Taarifa kwa Umma tarehe 6 Januari, 2024 ya kusitisha leseni na ratiba za mabasi 35 ya *Kilimanjaro Truck Company Limited* kuanzia tarehe 8 Januari, 2024. Hatua hii ilitokana na ukiukwaji wa masharti ya leseni uliofanywa na Mtoa Huduma, hususan kutoa huduma bila kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao (*e-Ticketing System*) na kutoza nauli zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa na LATRA. Kampuni ilitakiwa kutekeleza masharti iliyopewa ikiwemo kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao, kuzingatia viwango vya ukomo wa nauli vilivyowekwa na LATRA pamoja na kuwasilisha maombi ya kurejesha huduma ambayo itaiwezesha LATRA kuhakiki mfumo wa Tiketi Mtandao, nauli zilizoingizwa kwenye mfumo na madaraja ya mabasi hayo 35 kabla ya kuruhusu leseni na ratiba za mabasi husika kuendelea kutumika.

Baada ya Kampuni kukamilisha maelekezo ya LATRA na kuwasilisha maombi ya kurejesha huduma, LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, pamoja na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu (NIDC), imehakiki mfumo wa Tiketi Mtandao wa *Kilimanjaro Truck Company Limited*, nauli zilizoingizwa kwenye mfumo, ubora wa mabasi na madaraja kisha kuyawekea stika za utambulisho wa madaraja ili iwe rahisi kwa abiria kutambua daraja la basi kwa nauli anayolipa.

LATRA inapenda kutoa Taarifa kwa Umma kwamba imeruhusu leseni na ratiba za mabasi 35 ya *Kilimanjaro Truck Company Limited* kuendelea kutumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Orodha ya mabasi hayo 35 imeambatishwa kwenye Tangazo hili.

Kupitia Tangazo hili, tunawakumbusha watoa huduma wote wa mabasi yaendayo mikoani kuhakikisha mabasi yao yanabandikwa stika za madaraja (***Luxury Bus, Semi-Luxury Bus*** na ***Ordinary Bus***). **Stika hizi zimetengenezwa kwa gharama za Serikali.** Daraja la *Semi-Luxury* lina *Upper Semi-Luxury* na *Lower Semi-Luxury* lakini nauli zao hazitofautiani. Nauli ya daraja la *Ordinary Bus* ni ya chini kuliko nauli ya daraja la *Semi-Luxury Bus*.

Imetolewa na:

Habibu J. S. Suluo

MKURUGENZI MKUU

14 Januari, 2024



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI**



MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

**ORODHA YA MABASI 35 YA *KILIMANJARO TRUCK COMPANY LIMITED*
YALIYORUHUSIWA KUENDELEA KUTUMIA LESENI NA RATIBA ZAKE
KUANZIA TAREHE 14 JANUARI, 2024**

Na	Namba ya Usajili	Njia (Route)	Leseni ya LATRA
1	T491ARB	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A214433
2	T165DMH	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213378
3	T772ADJ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213017
4	T830AXR	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213822
5	T676DHY	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A213237
6	T805DDB	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213277
7	T689DHY	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212037
8	T893APD	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A214001
9	T814BGZ	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A213494
10	T545BHY	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212786
11	T639AQN	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213992
12	T278ALQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212248
13	T860BVA	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A3A290396
14	T708DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213427
15	T163DMH	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213389
16	T540AQK	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213877
17	T675DHY	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A213258
18	T705DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A211656
19	T855AXR	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213854
20	T804DDB	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A211889
21	T895APD	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213676
22	T709DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213619
23	T622DPT	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213021
24	T983AWY	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A214099
25	T904ACN	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A212137
26	T546BHY	DAR ES SALAAM - NAMANGA	A4A212365
27	T178EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213841
28	T176EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213856
29	T173EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213878
30	T177EAU	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213866
31	T832ASM	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213855
32	T434DKL	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A211949
33	T809BGZ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213846
34	T871BVA	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A3A289383
35	T706DGQ	DAR ES SALAAM - ARUSHA	A4A213650